# Mtazamo wa Karibu—Ushirikishi na Kutenga

Chaguo la kufuatilia mkakati wa ushirikishi au uwekezaji wa kutenga—ambao mara nyingi huitwa kuondoa uwekezaji—ni mjadala wa muda mrefu kati ya wawekezaji endelevu.

## Je, Kushirikisha au Kuondoa Uwekezaji?

**Ushirikishi** ni wakati tunapotumia ushawishi wetu kama mwekezaji kuweka mazungumzo ya kujenga na kutoa mapendekezo yanayoleta mabadiliko kati ya makampuni, watunga sera na wasimamizi wa mali.

**Kuondoa Uwekezaji** ni wakati mwekezaji anauza mali yake katika aina fulani ya uwekezaji. Wawekezaji wanaweza kuondoa mali zao kwa sababu wanaamini kwamba uwekezaji fulani hauambatani na maadili yao au unaleta hatari fulani ya kifedha.

Katika Wespath, tumejitolea kwa ustawi wa kifedha wa kudumu kwa washiriki wetu na wateja wa taasisi hii.
Tunaelewa umuhimu wa kimaadili na kifedha wa kuendeleza maendeleo katika masuala ya uendelevu, na kwa muda mrefu tumehisi kwamba ushirikishi ni chombo bora zaidi cha kufanya hivyo.

## Utafiti Kadhaa Wakielimu Unaunga Mkono Ushirikishi:

"Tunaonyesha kuwa katika ulimwengu wenye ushindani kuondoka (kuondoa uwekezaji na kususia) hakuna ufanisi kuliko sauti (ushirikishi) katika kusukuma makampuni kutenda kwa njia ya kuwajibika katika jamii."
– *Watafiti wa Harvard, Chuo Kikuu cha Chicago na Chuo Kikuu cha Trento (Italia)*[1]

"Kwa hivyo, uwekezaji endelevu unaoondoa mtaji kutoka kwenye kampuni za kahawia na kuupeleka kwenye kampuni za kijani unaweza ukawa na matokeo kinyume, kwa kuwa unafanya kampuni za kahawia kuwa za kahawia zaidi bila kufanya kampuni za kijani kuwa kijani zaidi."
– *Watafiti wa Chuo cha Yale na Boston*[2]

"(Kampuni zinazozalisha mafuta, gesi na nishati) zinazalisha kwa wingi, na kwa ubora wa hali ya juu zaidi, uvumbuzi wa kijani. Katika sehemu nyingi za teknolojia ya kijani, zinaonekana kuwa washawishi wakubwa wa kwanza, wasioweza kubadilishwa kwa urahisi."
– *Harvard, Chuo Kikuu cha Texas-Dallas na watafiti wa Chuo Kikuu cha DePaul*[3]

Utafiti huu unakamilishwa kwa historia ndefu ya miongo mingi ya Wespath, ambayo imeleta mafanikio mengi katika sekta na masuala ya uendelevu.

## Kushirikisha Sekta ya Mafuta na Gesi kwenye Mpito wa Hewa Mkaa wa Chini

Wespath ina ushirikiano wa miaka mingi na **Chevron** na **Occidental Petroleum (Oxy)**. Kushirikisha kumesababisha matokeo mazuri yafuatayo:

- Makampuni yote mawili yanachapisha ripoti zao za kwanza kabisa za hatari ya tabia-nchi, na kutoa kauli muhimu ya kutambua hadharani athari ya mabadiliko ya tabia-nchi.[4]
- Oxy ni kampuni kubwa ya kwanza ya mafuta na gesi kutangaza lengo la kufikia utoaji wa hewa ukaa usiozidi sifuri.
- Chevron ni ya kwanza katika sekta hiyo kupendekeza kura kwa pendekezo la wanahisa linalolenga usimamizi wa methani, ambalo lilipita kwa uungwaji mkono wa 98%.

## Kushirikisha Bingwa wa Vifaa vya Ujenzi HeidelbergCement kuhusu Haki za Binadamu

Wespath ilikuwa imefanya ushirikiano wa moja kwa moja na kampuni kubwa ya vifaa vya ujenzi ya Ujerumani **HeidelbergCement** kuhusu hatari kwa haki za binadamu, lakini mazungumzo yalipovunjika, tuligeukia njia tofauti ya ushirikishi. Tuliwasilisha pendekezo pingamizi kwenye kampuni, sawa na kuwasilisha azimio la wanahisa kwenye kampuni ya Marekani. Tangu pendekezo pingamizi lilipowasilishwa, HeidelbergCement ilianza tena mazungumzo, ikaajiri afisa wa mipango ya haki za binadamu mwenye uzoefu na ilionyesha uwazi zaidi wa kuzungumza kuhusu minyororo yake ya ugavi.

**Simulizi zaidi za mafanikio ya ushirikishi zimefafanuliwa upande wa nyuma!**

# Ushirikishi wa Wanahisa–Simulizi za Mafanikio



*Lucas Schoeppner wa Wespath (picha kulia), Meneja wa Usimamizi Endelevu wa Uwekezaji, na wawekezaji wenzake wanatembelea kisima cha gesi asilia kama sehemu ya lengo letu la kupunguza methani, sehemu kuu ya gesi asilia.*

*Kupunguza uvujaji wa methani kutoka kwenye miundombinu ya mabomba ni ushindi kwa wote: Huhifadhi bidhaa zinazozalisha mapato kwa makampuni ambayo tunawekeza na kupunguza utoaji wa gesi chafuzi ya ukaa. Mbali na kuzungumza na kampuni za mafuta na gesi kuhusu sera zao za udhibiti wa methani, Wespath imeyashirikisha mashirika ya serikali kuu kwa kuandika barua za kuunga mkono viwango vinavyopendekezwa vya utoaji wa methani.*

Kwa taarifa zaidi, tembelea tovuti yetu ya Uwekezaji Endelevu:

## Kimazingira

Wespath inaongoza ushirikishi na **Cummins**, kampuni ya utengenezaji inayounda injini, jenereta na vipengele vya nishati. Pamoja na wenzetu katika shirika la Climate Action 100+, mpango mkubwa zaidi wa ushirikishi ulimwenguni, tumeihimiza Cummins kushughulikia uendelevu wa mazingira na mpito unaolekea kwa mtindo wa biashara ya kaboni ya hewa mkaa wa chini. Mwaka uliopita, wasimamizi walitangaza Destination Zero, mkakati wa kuoanisha biashara yao na mustakabali wa viwango vya hewa ukaa sifuri kufikia mwaka 2050.

Pia tunaonyesha uongozi wa ushirikishi wa maswala ya tabia-nchi kupitia kazi yetu na **Muungano wa Wamiliki wa Mali wa Net-Zero Asset**, unaofafanuliwa kama "kiwango cha dhahabu" kwa ahadi kuhusu tabia-nchi.[5]jarida la mabadiliko makubwa la Muungano huo, *The Future of Investor Engagement*, ambalo Wespath iliiandika kwa pamoja, linatoa muhtasari muhimu wa hatua ambayo wawekezaji wanaweza kuchukua ili kusaidia kufikia uchumi unaozalisha hewa ukaa sifuri kupitia ushirikishi wa wanahisa. Jarida limesambazwa sana na linafunzwa na programu za wasomi za MBA.

## Kijamii

Wespath inahimiza makampuni kufichua taarifa zinazohusiana na haki za wafanyakazi na watu walioathiriwa na shughuli za kibiashara. Katika mazungumzo na **Caterpillar**, tuliihimiza kampuni hiyo ishughulikie hatari za biashara zinazohusiana na matumizi ya bidhaa zake katika maeneo yenye migogoro, ikiwemo Sahara Magharibi, ambayo ni eneo lililotwaliwa na Moroko; Mkoa wa Xinjiang wa Uyghur; Maeneo ya Palestina yaliyotwaliwa; na Myanmar, ambako mapato kutokana na uchimbaji madini ya jade yamefadhili migogoro. Kwa kujibu, Caterpillar ilifanya tathmini kuhusu matokeo ya haki za binadamu katika vitengo vyake vyote na kuimarisha sera yake ya haki za binadamu.

Kufuatia ukiukaji wa mara kwa mara wa usalama wa kazini katika **Dollar General**, Wespath ilisaidia kuongoza mazunguzo na muuzaji rejareja wa gharama ya chini yaliyoangazia sera zake za usalama katika mahali pa kazi. Ushirikishi huo ulisababisha mwekezaji mshirika kuwasilisha azimio la wanahisa la kutaka ukaguzi huru. Wespath iliunga mkono pendekezo hilo, na lilipita kwa idhini ya wanahisa wengi kwenye jaribio la kwanza.

## Utawala

Utafiti unaonyesha[6] kwamba bodi zenye uanuwai huleta utendakazi bora. Wespath ni mwanachama wa **30% Coalition**, shirika ambalo linatetea uanuwai wa kijinsia kwenye bodi. Tangu mwaka 2012, zaidi ya kampuni 400 zimeongeza wanawake kwenye bodi zao kupitia juhudi za Muungano huu.[7]

Sisi ni viongozi wenza wa shirika la **Investors for Opioid & Pharmaceutical Accountability (IOPA)**. IOPA inaangazia mageuzi ya usimamizi wa mashirika ambayo yanakuza uwajibikaji wa shirika katika tasnia ya opioidi na dawa. Kufuatia ushirikishi wa IOPA, kampuni tano za dawa zilikubali kubadilisha mbinu zake za malipo ya watendaji ili kusaidia kuhakikisha viongozi wa shirika wanawajibishwa kwa hatua zinazochukuliwa na kampuni zao.

*Manufaa na Uwekezaji wa Wespath hutekeleza mikakati endelevu ya uwekezaji kwa ajili ya fedha za uwekezaji zinazopatikana kwa na kupitia kampuni tanzu zake za usimamizi wa uwekezaji, ikiwemo Uwekezaji wa Kitaasisi wa Wespath. Wespath na kampuni tanzu zake inajulikana kwa pamoja kama "Wespath."*

[1] Broccardo, Eleonora, na wengine. "Exit vs. Voice." Ofisi ya Taifa ya Utafiti wa Kiuchumi. Agosti 2020. https://doi.org/10.3386/w27710

[2] Hartzmark, Samuel, na Kelly Shue. "Counterproductive Sustainable Investing: The Impact Elasticity of Brown and Green Firms." Inapatikana kwenye SSRN. Novemba 1, 2022. https://dx.doi.org/10.2139/ssrn.4359282

[3] Cohen, Lauren, na wengine. "ESG-Innovation Disconnect: Evidence from Green Patenting." Ofisi ya Taifa ya Utafiti wa Kiuchumi. Oktoba 2020. https://doi.org/10.3386/w27990

[4] https://www.oxy.com/sustainability/; https://www.chevron.com/corporate-responsibility/climate-change

[5] https://www.unepfi.org/industries/investment/antonio-guterres-net-zero-asset-owner-alliance-is-gold-standard-for-net-zero-commitments/

[6] *CS Gender 3000*, Credit Suisse Research, Sept. 2016.

[7] http://www.30percentcoalition.org/